

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA TATU

05 MEI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA ISHIRINI NA TATU – TAREHE 05 MEI, 2021


I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MAJI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

III. MASWALI:



OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

190. MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI
CHAUREMBO (MBAGALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi,
Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuipa fedha Halmashauri ya Temeke ili iweze kujenga Shule mpya za kutosha kutokana na Jimbo

la Mbagala kuongoza kuwa na Wanafunzi wengi wa Shule za Msingi na Sekondari.

191. MHESHIMIWA ALAUDIN HASHAM SALIM (ULANGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza barabara za Ulanga na kutenga bajeti ya dharura ili TARURA iweze kukarabati Barabara mara tu zinapoharibika;
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuipatia TARURA ya Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga usafiri ili kuongeza ufanisi katika kazi zao.

192. MHESHIMIWA JESCA JONATHANI MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itarekebisha tatizo la Hospitali ya FRELIMO ambayo inapata mgao kama Kituo cha Afya wakati ni Hospitali ya Wilaya ya Iringa tangu Mwaka 2013.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

193. MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN MANYANYA (NYASA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:

Je, kwa nini mikopo ya injini za boti isitolewe kwa mtu mmoja mmoja aliye tayari kuliko kutoa kupitia vikundi jambo ambalo linachelewesha ukuaji wa Sekta ya Uvuvi.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

194. MHESHIMIWA ANASTAZIA JAMES WAMBURA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, ni kwa kiasi gani eneo la EPZ lililotengwa na Mamlaka ya Bandari Mkoani Mtwara kwa ajili ya uwekezaji limetumika kwa shughuli iliyokusudiwa.

WIZARA YA KILIMO:

195. MHESHIMIWA ALLY ANYIGULILE JUMBE MLAGHILA (KYELA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-


Je, ni lini Serikali itaanzisha kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia Mto Songwe, Kiwila, Mbaka na Lufilyo ili kuongeza uzalishaji wa mpunga na kukuza uchumi wa nchi.

WIZARA YA NISHATI:

196. MHESHIMIWA ALI HASSAN OMAR KING (JANG'OMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro wa bei ya umeme unaotumika na Watanzania waishio Zanzibar ili kuweka usawa kwa Watanzania wote.



WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

197. MHESHIMIWA EMMANUEL MAGENI KASALALI (SUMVE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini barabara ya kutoka Magu – Kwimba hadi Ngudu itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami ili kuunganisha Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba na Makao Makuu ya Mkoa wa Mwanza.

198. MHESHIMIWA MOHAMED LUJUO MONNI (CHEMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi;

Je, ni lini Serikali itanza ujenzi wa barabara ya Handeni – Kiberashi – Kiteto – Mrijo – Chemba – Kwamtoro hadi Singida kwa kiwango cha lami kwa kuwa ipo kwenye Ilani na pia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais.

WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

199. MHESHIMIWA ALLY YAHYA MHATA (NANYUMBU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, ni lini changamoto ya mawasiliano ya simu Wilayani Nanyumbu itamalizika katika Kata za Likokona, Mkonona, Nangomba, Nandete, Napacho, Lumesure, Michiga na Chipuputa.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

(Majadiliano Yanaendelea)

**DODOMA
05 MEI, 2021**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**

